# Utandao Katika Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo
# (Networking in Savings and Credit Cooperative Societies)

**Mada Imetolewa Na**

**Prof. Suleman Chambo**

**Semina ya Vyama Vya Ushirika vya Akiba na Mikopo vya Utandao Wa Usawa Tarehe 7 Desemba 2009, Moshi, Tanzania**

## 1.0 UTANGULIZI

Miaka ya zamani, gari zima lilikuwa linatengenezwa na makampuni makubwa. Hivi şaşa, gari moja zuri na kubwa, linatengenezwa na makampuni mengi. Lakini gari linalotengenezwa na makampuni mengi ni kubwa na zuri mno kuliko lile lililokuwa linatengenezwa zamani. Sababu yake ni moja tu; yale makampuni madogo yamezamia katika utengenezaji wa vitu kimoja kimoja. Haya makampuni madogo madogo, yanafanya kazi kwa kutumia utandano. Utandano ni utaratibu mpya wa kiorgananizesheni, ambao huwa unaandaliwa kwa makusudi ili kuleta ufanisi katika shughuli yoyote ile ambayo wahusika wamepanga kuifanya.


Dhana ya utandao, imejaribiwa kwa mafanikio makubwa katika mashirika mbali, na vile vile imeingia katika taratibu za kuendeleza na kusimamia vyama vya ushirika vya Akiba na Mikopo, na vyama vya aina nyingine. Kwa mfano, kule Uganda, vyama vya ushirika vya kuuza mazao, baada ya miaka mingi ya ushindani kati ya vyama vya msingi na vyama vikuu baada ya kuanzishwa kwa şoko huru, vilijinyumbua vikaanza kujipanga upya kwa mfumo wa utandao. Vivyo hivyo, mfumo wa ushirika wa vyama vya ushirika vya akiba na mikopo vya USAWA, nao unatumia taratibu za utandao. Nia ni kuleta ufanisi, nguvu na kuimarisha, kuitekeleza kanuni ya sita ya ushirika, yaani ushirikiano kati ya vyama vya ushirika.

Mada yetu inataka tutolee maelezo kuhusu utandao katika ushirika wa vyama vya ushirika vya Akiba na Mikopo.

İli kuichambua mada hii, tutagusia mambo makubwa manne: Kwanza utandao ni nini, pili tutazungumzia nadharia ya utandao katika vyama vya ushirika tukigusia nadharia tatu za maumbile ya mitandao ya ushirika pamoja na historia yake. Tatu tutazungumzia fursa za mitandao katika vyama vya ushirika wa Akiba na Mikopo na nne, tutazungumzia maisha ya baadaye ya mitandao ya ushirika wa vyama vya Akiba na Mikopo.

## 2.0 UTANDAO

Utandao maana yake ni utaratibu wa muundo mpya wa ki-asasi ambao watu au asasi wanajenga mfumo wa kuwasiliana na kushirikiana katika kutekeleza majukumu yanayoshabihiana na yaliyobainishwa kwa uwazi. Sura ya utandao iko kama uzi unaotengenezwa na mdudu aitwaye buibui. Au, ni utaratibu wa kiuongozi wa asasi ambao una mfumo wa nyavu za kuvulia samaki au kukamatia wanyama.




Utandao una sehemu mbili muhimu; Kwanza ni kituo na pili ni kiungo. Kituo kinaweza kuwa mtu mmoja mmoja, au asasi na kiungo, ni aina ya uratibu wa shughuli, mikataba au maridhiano yaliyokubaliwa na kutekelezwa na vituo husika. Vituo vinavyojenga utandao vinaweka bayana masuala na michakato ambayo kwayo, itaashiria kuwapo kwa utandao wa aina inayoweza kudhihirishwa. Kati ya vituo husika, kuna mawasiliano mengi yaliyo rasmi na yasiyo rasmi, ana kwa ana, au kwa njia nyingine za mawasiliano kama simu, au elektroniki. Mikutano mingi, sasa hivi, inaweza kufanyika kwa taratibu za mawasiliano ya simu za mkono, ujumbe mfupi au kwa kutumia mawasiliano ya ana kwa ana katika warsha au elektroniki na wavuti.

Kwa utaratibu wa namna hiyo, shughuli nyingi zinazofanywa na vituo husika, zinaweza kufanyanyika kwa ukubwa sana kwa muda mfupi na kwa faida kubwa. Kinachotakiwa ni kuwa na mambo machache ya muhimu ambayo vituo vinaweza kutekeleza bila kipingamizi, mabishano au vikwazo vya aina nyingi. Kanuni kubwa inayoongoza shughuli za utandao, ni **MARIDHIANO YA PAMOAJA**.

## 3.0 NADHARIA YA MITANDAO KATIKA USHIRIKA

Taratibu za utandao, zimetumika katika maongozi ya vyama vya ushirika tangu chimbuko lake miaka ya 1800. Chama cha ushirika kinapoanzishwa, wanachama wanakubaliana kufanya shughuli zao kwa taratibu za kiushirika. Uamuzi huu, tayari unaashiria, utandao kati ya mtu na mtu, au mwanachama na mwanachama. Ni lazima tutambue kuwa, makubaliano ya kuunda chama cha ushirika yanatokana na uamuzi wa wanachama kukubali kushirikiana kutekeleza jambo fulani kama binadamu katika jamii husika. Wanapofanya hivyo, wanatumia **mtaji wao jamii** na siyo fedha (Teodosio:2008). Ni muhimu kutambua kwamba kinachowavuta watu kuanzisha ushirika, ni nguvu za mtaji wa kijamii na siyo fedha.

Pindi, wanapokubaliana kuunda mtandao wa kushirikiana, hatua ya pili ni kuangalia mtaji wa **kifedha** walio nao, ili mtaji wao wa jamii uweze kuimarika. Wanapochanga fedha, wanatekeleza utaratibu wa kiuwezeshaji ili mtandao wao uweze kuimarisha na kupanuka. Baada ya kutekeleza utaratibu wa kuwekeza fedha, wanaandaa malengo yatakayotekelezwa na ushirika wao pamoja na kujiendeleza kijamii, kiuchumi na kitamaduni.

Katika sura ya kawaida ya ushirika wa aina yoyote ile, kuna nadharia mbili ambazo zinaashiria misingi ya uundwaji wa vyama vya ushirika.


Kwanza, ushirika unaundwa kama majibu ya matatizo ya kiuchumi na kijamii. Matatizo hayo yanaweza kuwa ya umaskini, uharibifu wa mazingira, magonjwa, na kadhalika. Kutokana na matatizo hayo yenye ukubwa wa kuikumba jamii, vyama vya ushirika huwa vinaundwa kutoa majibu ya matatizo hayo. Katika uundwaji wa vyama vya ushirika huwa kunatokea machimbuko ya aina mbili kuu. Chimbuko Ia kwanza ni kuundwa kwa chama cha ushrika kutokana na mchakato wa kielimu hadi wanaounda chama cha ushirika waelewe na kuyaelewa vizuri mazingira yao ya umasikini, Wanakuwa katika hali ya utayari wa kuunda chama cha ushirika kwa utashi wao na hiari yao. Ushirika huu unatokana na ridhaa ya wanachama binafsi na kila mmoja anajua **KINACHOTAKIWA KUFANYWA NA KILA MWANACHAMA KWA FAIDA YA USHIRIKA WAKE NA FAIDA YAKE BINAFSI** Vyama vinavyoundwa kwa utaratibu na mchakato wa aina hii, vinafahamiana na malengo yao vinayajua na vinaweza kukabili vikwazo vya aina mbali mbali na kuvimudu kwa sababu ya ubora wa aina ya wanachama wake na dhamira zake. Ushrika wa namna hii unaweza kujipanga hadi ngazi ya kitaifa na unajulikana kama **ushirika nguvu moja**

Lakini uko ushirika ambao mchakato wake unategemea amri kutoka juu. Wakati mwingine serikali inaweza kuona ushirika wa aina wa aina fulani ni mzuri na una manufaa kwa wananchi wake. Kwa kuona umuhimu huo, na badala ya kuelimisha wananchi, inatoa amri kwamba, kuanzia tarehe fulani, wananchi wote wajiunge katika vyama vya ushirika kwa sababu vina faida kubwa. Watu wanaweza kujiunga katika ushirika huo kwa sababu wametakiwa na serikali kufanya hivyo na labda kwa kutekelwza sera za maendeleo za serikali au kuimarisha ugawaji wa mafao fulani kwa wananchi.Ushirika wa namana hii ukiundwa kitaifa unaitwa **ushirika sambaza**

Swali kubwa amabalo tunaweza kujiuliza ni je ushirika tulio nao leo hapa Tanzania ni ushirika nguvu moja au ushirika sambaza? Swali hili nawaachieni mlijibu wenyewe.

Nadharia ya pili ni ya maumbile ya ushirika kitaifa. Kuna mifumo miwili ya utandao wa Ushirika. Kwanza ni mfumo **msonge** na mfumo **lala.** Mifumo yote hii inatumika hapa Tanzania. Katika mfumo msonge, vyama vya ushirika vya msingi, vinaunda vyama vikuu, na baadaye vyama vikuu vinaunda vyama vya kilele na shirikisho. Vingine vinaanzia na vyama vya msingi hadi chama kilele kitaifa. Hii ni mitanda , lakini ina umbile Ia msonge.

**MCHORO 1: MUUNDO MSONGE WA MTANDAO WA USHRIKA**




Mfumo lala vile vile uko Tanzania. Mfumo huu, una maumbile ya utandao ambao **UMELALA** au **MDUARA**. Mara nyingi unajikita katika kufanya shughuli kwa ushirikiano wa karibu zaidi. Mara nyingi vile vile mtandao huu, unaunda chombo cha kati ambacho kinapewa majukumu machache, lakini ya muhimu ambayo hayawezi kufanywa na chama kimoja kimoja peke yake. Mambo hayo ni pamoja na uhasibu, ukaguzi wa ndani, kujenga mfumo wa teknolojia ya kupeana taarifa kwa kutumia njia za kisasa hasa za tovuti. Vyama hivi vinaweza kufungua website yao ambayo vinaweza kuitumia kutekeleza mambo yao mengi pamoja na kufanya maamuzi ya pamoja. Kwa kufanya hivyo, ushirika huu unaweza kufanya kazi kwa ufanisi wa hali ya juu na kupunguza gharama za uendeshaji.

Hata hivyo, pamoja na kwamba utandao huo unaweza kuwa na fursa ya kujenga ushirika wa nguvu moja, ni rahisi vile vile ukawa na tabia ya ushirika sambaza.

## 4.0 FURSA ZA UTANDAO LALA KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO

Utandao una fursa nyingi katika vyama vya akiba na mikopo. Kwanza kama ilivyoainishwa, utandao katika vyama vya ushirika, ni utekelezaji wa kanuni ya sita ya ushirika ya kushirikiana nkwa vyama vya ushirika kijamii, kitaifa na kimataifa. vyama vya ushirika vinapofanya kazi kwa mtandao, vinajenga fursa ya ushirika nguvu moja. Pili, ni rahisi kutumia taaluma adimu bila gharama kubwa. Kwa kutumia chombo cha kati. vyama vya akiba na mikopo vinavyotumia utandao, vinaweza kuajiri

wataalam wachache muhimu wakawatumia kwa gharama nafuu. Tatu, ni rahisi kuiga ufanisi ambao unatumiwa na vyama vinavyoendeshwa vizuri ambavyo ni washiriki kwenye mtanadao. Nne, ni rahisi kupata mawasiliano kuhusu teknolojia mpya ya kuleta ufanisi wa shughuli. Tano ni rahisi kuleta ubunifu wa kubiashara na kuongeza tija kwa wanachama wakati wote. Sita ni rahisi kuleta miongozo ya utawala bora kwa sababu vyama vyote vinafanya kazi kwa kutumia taratibu za aina moja za kiutawala na kimenejimenti kwa misingi ya uwazi, uwajibikaji, kutabirika na uanachama shirikishi najasirishi. Saba ni rahisi kutambua vyama vyenye matatizo kwenye mtandao, kuliko vyama vinavyofanya kazi kimoja kimoja peke yake. Vile vile ushirika mtandao lala, unaleta fursa ya vyama na wanachma wake kufahamiana vizuri na kuimarisha mtajijamii wa ushirika wao badala ya kufanya shughli za fedha tu.

## 5.0 MAISHA YA BAADAYE YA UTANDAO KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA VYA AKIBA NA MIKOPO

Kama tulivyosema kuwa utandao ni dhana mpya katika ushirika. Dunia nzima hivi sasa inaelekea kwenye mifumo ya utandao ya aina mbali mbali. Ndiyo maana nchi nyingi hivi sasa zinaongozwa kwa kutumia mitandao ya aina mbali mbali, kwa mfano Jumuiya ya Ulaya, Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na ile ya Magharibi. Kwa ufupi, dhana ya ushirika na kufanya kazi kwa mitanadao, imekuwa ni kawaida na ndiyo kimbilio la nchi na asasi nyingi kama zinataka kuishi na ushindani wa kibiashara katika dunia ya utandawazi na kushinda.

Lakini je, vyama vya ushirika vina changamoto gani ili utandao uweze kufanikiwa kuviweka katika soko?

Kwanza ni uogozi ulioelimika na imara. Vyama vya ushirika vinategemea sana uongozi wa kidemokrasia na kibiashara. Mara nyingi, uongozi umehusishwa sana na demokrasia na biashara wameachiwa waajiriwa. Hii haileti tija katika vyama vya ushirika kwa sababu, viongozi wa vyama vya ushirika wanatakiwa wawe mahiri vile vile katika biashara ya ushirika. Pili, chombo cha kati kuanza tabia ya ukiritimba wa kiutawala. Nİ rahİsİ kwa mitandao ya ushirika kutumia huduma za chombo cha kati na kupunguza gharama na kwahiyo kushindana vizuri katika şoko huru. Lakini inaweza kufika wakati, vyombo vya kati vikaanza tabia ya kujiona kuwa ni muhimu kuliko vyama wanachama wa mtandao. Hii inatokea kama elimu haitolewi kwa wanachama na hakuna uwazi katika shughuli za ushirika. Tatu ni pale ambapo vyama vyenye maendeleo makubwa katika mtandao vitakapojiona kuwa ni maarufu na kuwa ushiriki wa vyama vingine kwenye mtandao, ni mzigo mkubwa kwao. Tano ni pale ambapo kwa sababu ya kufuata kanuni za pamaoja na utekelezaji

Wake, vyama wanachama wa mtandao vikaanza kujiona kuwa vinatawaliwa na chombo cha kati na ya kwamba vinaanza kupoteza uhuru wa kujiamulia mambo yao vyenyewe.

Changamoto hizi ni za msingi, na zipo katka vyama wanachama wa mitandao ya ushirika. Wakati mwingine kwa utamaduni wa kuwa tegemezi huwa inaleta hisia kuwa vyama vya ushirika vinaundwa ili kuwa ndiva za kukusanya na kupokea misaada kutoka kwa wafadhili. Na ni rahisi kuuona ushauri kutoka kwa wataalam kuwa ni wa kujenga mitandao ya ushirika tegemezi na sambaza. Vile vile mazingira ya sheria ya ushirika yamekuwa kikwazo kuruhusu uhuru wa mitandao ya aina mbali mbali ya ushirika. Hii ni kwa sababu sera na sheria, pengine zinazungumzia mitandao finyu ya ushirika nısonge kwahiyo inapokuja mitandao ambayo haiku kweye sera na Sheria, imekuwa ikikwama kwa sababu ya kukosa ubunifu wa mamlaka husika.

**7.0 NINI KIFANYIKE**

Kipindi cha ushindani katika şoko kinachokuja ni kigumu sana. Sehemu tatu za ushindani zinazokokuja katika şoko la fedha ni ushinadani katika bidhaa za mawekezo, ushindani katika bidhaa za Mikopo, ushindani katika umahiri wa uongozi adilifu na jasiriamali. Lakini vile vile tunahitaji wanachama wajasiriamali na waadilifu katika kusimamia utawala bora. Kuna haja vile vile kuutumia kikamilifu utandao tuliouanzisha, tuukosoe mara kwa mara ili tuujenge upya kwa manufaa ya wanachama.

Mambo muhimu ya kufanya ni kama ifuatavyo:

Kwanza tunahitaji elimu kwa wanachama. Ushirika unatambua kuwa elimu kwa wanachama , ni mtaji mkubwa sana wa kisiasa na kiuchumi. Wanachama walioelimika, wanaweza kuhoji mambo mengi amabayo yanaletwa kwa hujuma au kısa hila. UJwezo Wa kutambua sera na sheria nzuri utatokana na wanachama. Vile vile , wanachama wanahitaji elimu ya uongozi , biashara na staid za ujasiriamali. ibaİnİke kuwa vyama vya ushirika vya akiba na mikopo, ni daraja la kufikia malengo ya kiuchumi, kiajamii na kiutamaduni ya wanachama. Kwa mantiki hiyo, ujasiriamali kwa wanachama wa vyama vya ushrika wa akiba na mikopo, uanaanzia kwenye shughuli za kiuchumi au huduma wanazozalisha na kuziuza katika soko. Shughuli za kilimo biashara, biashara ya kuuza bidhaa za viwandani, huduma na shughuli zo zote zile rasmi. Wote wanahitaji elimu kuanzia huko.

Pili ni kuongeza kiwango cha taaluma za weledi (Professional training) kwa watendaji wa vyama vya ushrika wa akiba na mikopo. Watendaji wa vyama na wale wa chombo cha kati, wanahitaji mafunzo ya hali ya juu ili wawe na silaha za kisasa za ushindani katika biashara. Wanatakiwa wapate

elimu ya juu katika uendeshaji wa vyama vya ushirika vya akiba na mikopo. Wanatakiwa wawe na mbinu mpya za kufanya utafiti wa şoko la bidhaa za vyama vya ushirika na kuziuza kwa wanachama na wateja wengine wa huduma za vyama vyao. Wanatakiwa walifahamu vizuri şoko la fedha linavyokwenda na kuwaarifu wanachama kuhusu şoko hilo na tabia yake. Viongozi na watendaji wanatakiwa wawe wabunifu wa bidhaa na mifumo mbali mbali ambayo itawaweka wanachama katika ufahamu mkubwa kuhusu umuhimu wa vyama vya ushirika vya akiba na mikopo.

Tatu tunahitaji maamuzi ya kijasirialamli na kijasiri kuhusu uwekezaji hasa katika teknolojia ya kompyuta. Ni katika uwekezaji wa namna hii, utatuwezesha kuimarisha vyama na mitandao yake kwa pamoja.

## 8.0 HITIMISHO

Utandao ni mfumo mpya wa menejimenti ya kitaasisi na mbinu mpya ya utawala ambayo itatumiwa vizuri na vyama vya ushirika badala ya mashirika ya watu binafsi ingawa yanautumia. USAWA ni aina ya utandao unaotumiwa na vyama vya ushirika vya akiba na Mikopo vya Kilimanjaro. Utandao una kanuni zake na viwango vyake. Kanuni kubwa ya utandao katika vyama vya akiba na mikopo ni maridhiano ya wanachama wote, elimu kwa wanachama, na mafunzo ya hali ya juu kwa mameneja.

Haya hivyo, ili USAWA uweze kufikia viwango vya ushirika nguvu, ni muhimu utandao huo ukaendeshwa kwa kupitia mtandao wa kompyuta na tovuti

## REJEA

Teodosio, et al. Social Capital Co-operatives and National Transformation. UNESCO, Philippines, 2008